Toleo Na.: 004

# JARIDA LA USHIRIKA

ISSN 2714 - 2175

OKTOBA - DESEMBA, **2020**

## VIONGOZI WA USHIRIKA NI LAZIMA TUBADILIKE,KUWASAIDIA WATANZANIA WENZETU WANYONGE – WAZIRI MKUU








*"Ushirika - Pamoja Tujenge Uchumi Imara na Endelevu"*

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| 2 | Kutoka kwa Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika |
| 3 | Salamu za Pongezi |
| 5 | Waziri Mkuu Apokea Taarifa ya Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Vyama Vikuu vya Ushirika vya NCU, KNCU NA SHIRECU |
| 6 | Serikali Yarejesha Mali za Bilioni 61 kwa Vyama Vikuu vya Ushirika |
| 8 | Serikali Imedhamiria Kuimarisha Benki ya Ushirika Nchini |
| 9 | Viwanda vya Ushirika Vyaongeza Bei Pamba Kumnufaisha Mkulima |
| 11 | Ushirika Afya – Bima Ya Afya Inayomlenga Kumnufaisha Mkulima |
| 12 | Mifumo ya Kuwezesha Upatikanji wa Fedha kwa Vyama vya Ushirika wa Nyumba |
| 14 | Taratibu za Uingiaji wa Mikataba Katika Vyama vya Ushirika |
| 15 | Viongozi wa Ushirika Mkoani Kagera Wapewa Mafunzo |
| 17 | Maswali na Majibu Kuhusu Mikutano Mikuu ya Wanachama wa Vyama vya Ushirika |
| 18 | Ushirika Unajengwa na Viongozi Walio Tayari Kujitolea |
| 20 | Madiwani Wapigwa Msasa Dhana ya Ushirika |
| 23 | Elimu ya Ushirika Iwafikie Wanachama Wote - Naibu Mrajis |
| 24 | Elimu ya Fedha Kuimarisha Ushirika Nchini |
| 25 | Tanesco Saccos Kujenga Jengo la Ofisi |
| 27 | Wanawake wahamasishwa Nafasi za Uongozi wa Ushirika |

# KUTOKA KWA MRAJIS NA MTENDAJI MKUU WA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA



**Dkt. Benson Ndiege**
Mrajis wa Vyama vya Ushirika na
Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania

## Mali Zilizorejeshwa Zitasimamiwa na Kutumika kwa Manufaa ya Wanaushirika

SERIKALI imerejesha mali mbalimbali za baadhi ya vyama vya ushirika nchini, ambazo zilichukuliwa bila kufuata Sheria na kumilikiwa na wajanja wachache wakiwemo viongozi wa vyama hivyo wasiokuwa waaminifu. Vyama vya Ushirika vya Nyanza (NCU), Geita (GCU), Simiyu (SIMCU) na Shinyanga (SHIRECU) vimerejeshewa mali zenye thamani ya Sh. bilioni 61 zilizokuwa zikimilikiwa kinyume cha utaratibu.

Tunapongeza uamuzi huu wa Serikali wa kurudisha mali za ushirika kwa Vyama vya Ushirika kwa kuwa mali zilizorejeshwa zitasaidia kufufua na kuimarisha utendaji kazi wa vyama vya ushirika nchini. Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) itahakikisha mali zilizorejeshwa zinatumika kwa manufaa ya wanaushirika na wakulima kwa ujumla ili ziwasaidie kuondokana na umasikini wa kipato.
Aidha, tunapongeza urejeshwaji wa mali za Vyama vya Ushirika kwa wanaushirika kwa kuwa wizi, ubadhirifu na matumizi mabaya ya mali ya vyama hivyo vilikithiri, kiasi cha kuviacha vyama vya ushirika katika umaskini mkubwa na kuharibu taswira ya Ushirika nchini.

Tunaipongeza Timu iliyoundwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kasim Majaliwa, kufuatilia mali zilizoporwa za Vyama vya Ushirika, ambapo Timu hiyo imefanikiwa kurudisha mali mbalimbali vikiwemo viwanja. majengo, vipuri pamoja na nyumba ambazo zilikuwa mali halali za Vyama hivyo.

Vongozi wa Vyama vya Ushirika vilivyorejeshewa mali wanatakiwa kuzitunza ili zisiweze kurudi tena mikononi mwa watu binafsi, Pamoja na kuhakikisha wanaushirika wananufaika na mali zao, Vilevile, viongozi wa vyama vya ushirika wahakikisha mali zilizorejeshwa zinatumika kwa manufaa ya wanaushirika na wakulima kwa ujumla ambao ndio wamiliki.

Timu ya Uchunguzi imebainisha kuwa waliohusika kufilisi mali za wanaushirika ni viongozi na watendaji wa vyama hivyo, ambao baadaye walijimilikisha wenyewe na kuwaacha hoi wanachamaTunaamini hatua za kisheria zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya viongozi hao na wengine watakaojihusisha na kuviibia Vyama vya Ushirika.

Mali za Vyama vya Ushirika Lazima zirudi, hata kama waliochukua walishaondoka kwenye madaraka, kama wako Tanzania hii na wako hai, lazima warudishe mali za wanachama. Serikali itaendelea kuwafuatilia waliohujumu Vyama vya Ushirika mahali popote walipo na kurudisha mali hizo kwa wanachama, ili kuwarejeshea nguvu ya kiuchumi wanaushirika kwa kuwa Ushirika ndio tegemeo kubwa kwa maendeleo ya wakulima, wafugaji na wavuvi.

# SALAMU ZA PONGEZI

**WIZARA YA KILIMO**
**TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)**

## Salamu za Pongezi



**Mhe. Prof. Adolph F. Mkenda**
Waziri wa Kilimo



**Mhe. Husein M. Bashe**
Naibu Waziri wa Kilimo

**TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)**
Tunaungana kuwa pongeza
**Mhe. Prof. Adolph F. Mkenda,** Kwa Kuteuliwa kuwa Waziri wa Kilimo
na **Mhe. Husein M. Bashe,** Kuwa Naibu Waziri wa Kilimo

*"Ushirika – Pamoja Tujenge Uchumi"*

@ushirika_tcdc ushirika_tcdc Tume ya Mendeleo Ushirika

# SALAMU ZA PONGEZI

WIZARA YA KILIMO
**TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA**

## SALAMU ZA PONGEZI



*Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli*



*Mhe. Samia Suluhu Hassan*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) inapenda kumpongeza Rais, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli na Makamu wa Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi na kuweza kutetea kiti cha Urais katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 2020.

TCDC inawahakikishia ushirikiano wa dhati katika kuunga mkono juhudi za mageuzi ya kiuchumi yanayolenga kukuza maendeleo jumuishi ya Taifa letu.

Ujasiri, dhamira ya kweli na utumishi uliotukuka wa Dkt. Magufuli na Mama Samia Hassan katika kutanguliza maslahi ya Taifa vimenufaisha Watanzania wengi katika kipindi cha miaka mitano ya mwanzo.

***Ushirika-Pamoja Tujenge Uchumi Wenye Nguvu Zaidi***

www.ushirika.go.tz ushirika@ushirika.go.tz ushirika_tcdc
@ushirika_tcdc Tume ya Mendeleo Ushirika

CS Scanned with CamScanner

# WAZIRI MKUU APOKEA TAARIFA YA UFUATILIAJI WA MWENENDO WA VYAMA VIKUU VYA USHIRIKA VYA NCU, KNCU NA SHIRECU



*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa akipokea Taarifa ya Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Vyama Vikuu vya Ushirika vya NCU, KNCU na SHIRECU kutoka kwa Kiongozi wa Timu Maalum ya Uchunguzi aliyoiunda, Asangye Bangu*

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kasim Majaliwa, Novemba 30, 2020 alipokea Taarifa ya utuatiliaji wa mwenendo wa vyama vya ushirika vya NCU (1984) Ltd, KNCU (1984) Ltd na SHIRECU (1984) Ltd kutoka kwa Timu maalum ya uchunguzi aliyoiunda.

Katika hafla hiyo, Waziri Mkuu amewataka viongozi wa vyama vya ushirika nchini wabadilike na wawe na weledi ili kurejesha heshima ya ushirika nchini. "Viongozi wa ushirika ni lazima tubadilike. Nyie mliopewa dhamana kwenye vyama vikuu hivi vitatu vya KNCU, NYANZA na SHIRECU lazima mbadilike, nyie mmepewa dhamana ya kuwasaidia Watanzania wenzetu wanyonge wanaolima ekari moja, mbili au tatu," amesisitiza Waziri Mkuu Majaliwa.

Mapema akiwasilisha taarifa hiyo mbele ya Waziri Mkuu, Kiongozi wa Timu hiyo maalum, Asangye Bangu, alisema Timu hiyo imefanikiwa kurejesha mali 60 za ushirika zenye thamani ya Shilingi bilioni 68.98. Mali hizo zinajumuisha majengo, viwanja, magari na mitambo ya machine, hazikuwa mikononi mwa vyama hivi vitatu lakini sasa zimerudishwa kwenye vyama hivyo.

# SERIKALI YAREJESHA MALI ZA BILIONI 61 KWA VYAMA VIKUU VYA USHIRIKA


Serikali ya Awamu ya Tano imefanikiwa kurejesha mali za vyama vikuu vya ushirika Nyanza, Geita na Simiyu zenye thamani ya Shilingi Bilioni 61 zilizokuwa zikimilikiwa kinyume cha utaratibu.

Akikabidhi hati 37 kwa wenyeviti wa vyama vya Nyanza (NCU), Geita (GCU) na Simiyu (SIMCU) mwezi Novemba, 2020 jijini Mwanza, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, amesema kazi hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya Mhe. Rais. Dkt.John Pombe Magufuli aliyoyatoa mwezi Agosti mwaka 2016.

“Leo nimekabidhi hati miliki 37 zinazojumuisha ardhi, majengo na mitambo yenye thamani ya shilingi Bilioni 61 zilizoporwa kinyemela na watu kutoka vyama vya ushirika Nyanza, Geita na Simiyu ambao ndio walikuwa wamiliki halali” alisema Kusaya.

Kusaya aliongeza kusema kazi hiyo ya kufuatilia na kurejesha mali imefanywa na Timu Maalum iliyoundwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa mwaka 2016 baada ya agizo la Rais Magufuli alipofanya ziara mkoani Mwanza kuwa mali zote za Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza zifuatiliwe na kurejeshwa toka kwa waliozimiliki kinyume cha utaratibu.

Ili kuhakikisha wanaushirika wananufaika na mali zao Katibu Mkuu Kusaya ametoa maagizo kwa viongozi wa vyama vya ushirika nchini kuwa kurejeshwa kwa mali hizo zitumike kwa manufaa ya wakulima ambao ndio wamiliki.




*Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Bw. Gerald Kusaya akikabidhi hati za NCU kwa Mwenyekiti wa NCU Mkoani Mwanza, Benjamin Mikomangwa, wakati wa Makabidhiano ya Mali zilizokuwa zimechukuliwa na watu binafsi bila kufuata utaratibu*

Pili, Mrajis wa Ushirika nchini ahakikishe mali zilizorejeshwa zinakuwa salama na kuwa asitokee kiongozi yeyote atakayefanya ubadhirifu.
Tatu, kwa watu wote ambao bado wanamiliki zilizokuwa mali za ushirika kinyume cha utaratibu wazirejeshe mara moja kwa serikali kabla hatua za kisheria hazijachukuliwa kupitia Timu Maalum ya Waziri Mkuu.

"Nyanza kuna jengo lipo Nansio Ukerewe linaitwa Pamba Hostel imebainika mkataba wake na Saad Songolo ulikiukwa. Tunataka lirudishwe Serikalini, hivyo Mkuu wa Mkoa wa Mwanza tunaomba uruhusu vyombo vya dola vifanye kazi yake ili mali hii ya wakulima irejeshwe" alisema Kusaya.
Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mwanza John Mongela ametoa pongezi kwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwa uthubutu wao na uzalendo wa kutaka mali zote za wanashirika zilizochukuliwa kinyemela kurejeshwa kwa wamiliki ambao ni wakulima.

Mongela alisisitiza kuwa mkoa wa Mwanza tangu agizo lilipotolewa viwanja vya Furahisha tarehe 11 Agosti, 2016 umeshirikiana na Timu Maalum ya Waziri Mkuu kwenye ufuatiliaji na hatimaye kufanikiwa leo kurejesha mali hizi 27 za chama kikuu cha Nyanza na zingine za Simiyu na Geita.
"Leo tunamshukuru Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwajali wakulima, wafugaji na wavuvi wa nchi hii hata kuagiza uchunguzi wa mali zao zilizoporwa na wajanja wachache kwenye ushirika" alisisitiza Mongela

Katika hatua nyingine Mkuu wa mkoa wa Mwanza, Mhe. John Mongela, alimpongeza Mwenyekiti wa kwanza wa Timu Maalum ya Waziri Mkuu ambaye sasa ni Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Gerald Kusaya kwa kazi nzuri ya kufuatilia urejeshwaji mali hizo kazi iliyokamilisha na timu ya pili chini ya Asangye Bangu.
Aidha, Mongela ametoa onyo kwa Viongozi wa Nyanza Cooperative Union kuwa wasimamie vizuri mali hizi ili zisije tena kuuzwa kwa watu kinyume cha utaratibu na kuwa sasa Nyanza inatakiwa kuwa na Mtendaji Mkuu mwenye weledi na ujuzi wa kusimamia ushirika.



*Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Bw. Gerald Kusaya akikabidhi hati za mali za SHIRECU kwa Mwenyekiti wa SHIRECU Mkoa wa Shinyanga Bw. Lems Kulwa Jishanga, wakati wa Makabidhiano ya Mali zilizokuwa zimechukuliwa na watu binafsi bila kufuata utaratibu*

Mongela ameiomba wizara ya kilimo ifanye kazi ya kuhakikisha vyama vikuu vya ushirika vinapata na kuajili mameneja wakuu wenye weledi, taaluma, ujuzi na uadilifu kuongoza ushirika ili vijiendeshe kibiashara badala ya kutumia uzoefu usio na tija.
Akiwasilisha taarifa Mwenyekiti wa Timu Maalum ya Waziri Mkuu Asangye Bangu alisema mali hizo zilizorejeshwa ni sehemu ya zoezi endelevu la kufuatilia watu wote waliojimilikisha au kuuziwa zilizokuwa mali za ushirika kinyume cha utaratibu. Bangu alitaja mali zilizorejeshwa kwa vyama vikuu vya ushirika Nyanza kuwa ni 27, Geita 9 na Simiyu 2 zikiwamo viwanja, majengo na mitambo na kuwa timu yake inaendelea kufuatilia mali zingine kwenye vyama hivi na vingine ikiwemo Kilimanjaro (KNCU) Shinyanga (Shirecu) na maeneo mengine.
Akitoa shukrai kwa niaba ya wanaushirika nchini Mrajis wa Ushirika Dkt. Benson Ndiege alisema kurudishwa kwa mali za ushirika kutasaidia kufufua na kuimarisha utendaji kazi wa vyama vya ushirika nchini.
Dkt. Ndiege alisema atahakikisha mali zilizorejeshwa zinatumika kwa manufaa ya wakulima ili ziwasaidie kuondokana na umasikini wa kipato.

# SERIKALI IMEDHAMIRIA KUIMARISHA BENKI YA USHIRIKA NCHINI

Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuimarisha Benki ya Ushirika Kilimanjaro (Kilimanjaro Cooperative Bank Ltd – KCBL) kwa lengo la kuwaletea maendeleo ya kweli Watanzania na kuwapunguzia umaskini. Benki ya Ushirika Kilimanjaro (Kilimanjaro Cooperative Bank Ltd - KCBL) iliyozinduliwa rasmi Oktoba 19, 2020 baada ya Mkataba wa Makubaliano na CRDB Bank PLC ambayo imefanya Uwekezaji wa Shilingi bilioni Saba (7) kuimarisha utendaji wa Benki ya Ushirika.




*Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL), Dkt. Gervas Machimu, na Mwenyeki wa Benki ya CRDB, Ally Laay, wakionyesha Mkataba wa Uwekezaji kati ya CRDB Bank na KCBL.*

Dhamira ya kuimarisha Benki ya ushirika imetolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Bw. Gerald Kusaya alipofungua Kongamano la Uwekezaji kwenye Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) lililofanyika Jijini Dodoma.

Amesema Serikali ya awamu ya tano, inayoongozwa na Mh. Dk. John Joseph Pombe Magufuri – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imedhamiria kwa dhati kuleta maendeleo ya kweli kwa watanzania na kuwapunguzia umaskini. Hivyo, kuimarishwa kwa KCBL kutasaidia Serikali kufikia azima yake ikiwa ni pamoja na kuimarisha huduma za jamii na kuwaongezea kipato kupitia huduma za kifedha zitakazotolewa na KCBL kwa wananchi.

“Serikali ya awamu ya tano inatambua umuhimu wa Ushirika nchini na ndio maana inaendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha shughuli za ushirika nchini ikiwemo kuchukua hatua kwa wote wanaobainika kutumia vibaya mamlaka yao pamoja na kufanya ubadhirifu kwenye Vyama vya Ushirika nchini,” amesema Bw. Kusaya.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo amesema kuwa kuimarika kwa Benki ya KCBL kutatoa fursa kwa Vyama vya Ushirika pamoja na wananchi kwa ujumla kupata huduma za Kifedha kwa karibu zaidi. Amewahamasisha wanaushirika wote pamoja na wadau mbalimbali kutumia fursa hii ya uwepo wa KCBL kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma za kifedha nchini.

“Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania pamoja na Benki Kuu ya Tanzania, vitaendelea kutoa ushirikiano wa karibu kwenye Benki hii na kuhakikisha Benki inasimama na kutoa huduma zinazokusudiwa,” amesema Katibu Mkuu.

# VIWANDA VYA USHIRIKA VYAONGEZA BEI YA PAMBA KUMNUFAISHA MKULIMA

Katika msimu wa 2020/2021 chama Kikuu cha Ushirika cha KACU ltd kiliweza kununua jumla ya kilo 2,273,663 za pamba zenye thamani ya sh 2,049,347,370/= za wakulima kutoka Halmashauri za Ushetu, Msalala, Kahama mji, Nyang’wale na kishapu kwa wastani wa bei ya sh. 900/= kwa kilo. Chama cha KACU kilikuwa kinanunua kwa bei nzuri ukilinganisha na makampuni binafsi, hivyo kuongeza bei kwa mkulima. Wakati makampuni binafsi walipokuwa wakinunua shilingi 810/= kwa kilo, chama kilinunua shilingi 850/= kwa kilo na pale ambapo makampuni binafsi yalianza kununua shilingi 850/= kwa kilo, chama kilianza kununua kwa shilingi 900/=, hali kadhali makampuni yalipoanza kununua shilingi 900/= kwa kilo, chama kilifikia mpaka shilingi 950/=.

Chama Kikuu cha Ushirika Chato - CCU ltd kilinunua jumla ya kilo 4,312,680 za pamba kwa bei ya wastani wa sh 900/= kwa kilo zikiwa na thamani ya sh. 3,881,412,000/= kutoka katika Halmashauri za Chato, Biharamulo, Geita na Muleba.



*Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Zainab Tellack (kulia) wakiwa na Viongozi wengine kwenye uzinduzi wa Kiwanda cha kuchakata pamba cha KACU*

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo iliazimia kufufua viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika nchini. Katika kutekeleza azma hii Wizara ya Kilimo Kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini (TCDC) kwa kushirikiana na Benki ya Kilimo (TADB) ilifanya tathmini ya viwanda 28 vya kuchakata pamba ambavyo vilikuwa vimesinzia kwa muda mrefu. Baada ya tathmini hiyo, viwanda vitatu vya KACU, CCU na MBCU vilionekana kuweza kukarabatiwa kwa haraka na kuanza kuchakata pamba msimu 2020/2021. Aidha, hadi msimu kumalizika ni viwanda viwili ndiyo viliweza kuwashwa na kuchakata pamba; navyo ni kiwanda cha Kahama Cooperative Union ltd (KACU) na Chato Cooperative Union ltd (CCU). Kiwanda cha Mbogwe Cooperative Union ltd kilishindikana kuwawashwa kutokana na kuchelewa kwa mchakato wa kuchukuwa mkopo kutoka benki.

Chama cha Ushirika cha KACU ltd kiliweza kukopeshwa jumla ya sh. 4,650,959,543/= kutoka benki ya kilimo (TADB) ambapo kati ya fedha hizi, sh. 600,000,000/= ilikuwa ni kwa ajili ya kulipa deni TIB na sh.4, 050,959,543/= kwa ajili ya ununuzi wa pamba, uchakata pamoja na gharama za uendeshaji shughuli za kiwanda.
Aidha, hadi kufikia mwisho mwa msimu jumla ya sh.3,186,767,658/= tu ndio zilizotumika kwa ajili ya zoezi zima la ununuzi, uchakaji na usimamizi. Hadi sasa chama kimefanikiwa kurejeshwa mkopo wote ambao ulichukuliwa kwa ajili ya shughuli za kiwanda pamoja na riba.

Hadi kufikia sasa, chama kimechakata pamba yote ambayo ilikuwa imenunua na kupata robota 4,671 za pamba nyuzi zenye uzito wa kilo 853,362 na mbegu za pamba kilo 1,321,080.
Mapato yatokanayo na mauzo ya pamba nyuzi pamoja na mbegu za pamba ni sh 3,369,252,439, Zoezi la uchakatajiwa wa pamba umekamilika na kwa sasa hakuna shughuli za kiwanda zinazoendelea kutokana na hakuna mali ghafi za kuchakata.

Chama cha Ushirika cha CCU ltd kiliweza kuchukuwa mkopo wa sh. 4,464,680,730/= kwa ajili ya ununuzi wa pamba, ukarabati wa mitambo na Gharama za usimamizi zoezi zima la msimu. Hadi kufikia 24-12-2020 chama kimeweza kurejeshwa sh. 4,120,000,000/= baki ya mkopo bila riba ya 12% ni sh. 344,680,730/=. Aidha, chama kitamaliza kurejesha mkopo wake pale ambapo kitakuwa kimemaliza shughuli za uchakataji na mauzo. Hivi sasa uchakataji bado unaendelea.

Hadi kufikia tarehe 24-12-2020 chama kimechakata jumla kilo 3,947,185 na kuzalisha robota 8,345 ya pamba nyuzi yakiwa na uzito wa kilo 1,510,445 na pia mbegu za pamba zilizozalishwa ni kilo 2,369,980. Uchakataji bado unaendelea ambapo bado kilo 365,495 za pamba kumalizika.

Hadi kufikia tarehe 24-12-2020 jumla ya mauzo ya pamba nyuzi na mbegu za pamba yalifikia sh.5,437,208,685/= Ambapo bei ya wastani kwa pamba nyuzi ikiwa ni sh 3,100/= kwa kilo na wastani wa bei kwa mbegu za pamba ikiwa ni sh 550/= kwa kilo. NB: Jumla ya mapato tarajiwa baada ya kuuza bidhaa zote ni sh. 6,502,675,633/=, hivyo chama kina uhakika wa kupata faida kubwa baada ya malipo yote kukamilika ikizingatiwa tayari wamelipa mkopo kwa asilimia zaidi ya 95.

# USHIRIKA AFYA – BIMA YA AFYA INAYOMLENGA KUMNUFAISHA MKULIMA

Serikali ya Awamu ya Tano iliwaelekeza Viongozi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (National Health Insurance Fund – NHIF) pamoja na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (The Tanzania Cooperative Development Commission – TCDC) kukaa kwa pamoja na kusanifu bidhaa ya bima ya afya ambayo ingewafaa wakulima wa mazao matano ya kimkakati kwa kuanzia.

Mnamo mwaka 2018 NHIF na TCDC walikuja na bidhaa ya bima ya afya iitwayo Ushirika Afya. Bidhaa hiyo ilizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, katika Wilaya ya Kahama Mkoa wa Shinyanga. Ujio wa bidhaa ya Ushirika Afya ni sehemu ya jitihada za Serikali kutekeleza Mpango wa Afya kwa Wote (Universal Health Coverage –UHC). Ili mkulima aweze kujiunga na Ushirika Afya lazima awe mkulima wa moja wapo ya mazao matano ya kimkakati lakini pia shuruti awe ni mwanachama hai na mwaminifu wa chama cha msingi cha ushirika wa kilimo na masoko (AMCOS) kinachojihusisha na ukusanyaji na uuzaji wa mazao hayo.

Mwanachama wa chama cha ushirika anatakiwa kulipia kiasi cha Shilingi 76,800/- kwa mwaka kwaajili ya kupata huduma za matibabu yeye binafsi katika Hospitali za ngazi zote hapa nchini pasipo kuhitaji kuandkiwa rufaa. Aidha, mwanachama huyo anakuwa na nafasi moja ya kumuingiza mwenza wake (mke/mume wa ndoa), na nafasi nne za kuwaingiza wanawe walio chini ya umri wa miaka 18 au wazazi wake au wa mwenza wake. Gharama za kumuingiza mwenza wake au wazazi ni Shilingi 76,800/- kwa kila mmoja na kwa watoto ni Shilingi 50,400/-.




Afisa Ushirika wa Wilaya ya Magu, Richard Majalla anaelezea kazi ya urajisishaji wa wanachama wa vyama vya msingi vya ushirika wa pamba katika Wilaya ya Magu. Baada ya uzinduzi wa bidhaa ya Ushirika Afya kule Wilayani Kahama, wadau wakuu wa Ushirika Afya ambao ni NHIF, TCDC, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza – NCU (1984) Ltd kwa mkoa wa Mwanza walielekezwa kufanya uelimishaji na uhamasishaji kwa wanachama wa vyama vya msingi vya ushirika wa pamba kupitia mikutano mikuu na mijumuiko mingine ya wanaushirika hao.

Katika awamu hiyo matarajio yalikuwa ni kwamba mwanaushirika akishaelimishwa kuhusu umuhimu wa kujiunga na Ushirika Afya, angeridhia kukatwa fedha za kugharamia huduma hiyo wakati wa mauzo ya pamba ili fedha hizo zilipwe na chama chake cha msingi kwa NHIF na wao NHIF ndipo wamwingize kwenye huduma ya Ushirika Afya.

“Kwakuwa viongozi wakuu wa Serikali wanafahamu fika umuhimu wa wakulima hao kuwa na uhakika wa kupata matibabu bora ili wawe na afya njema, walielekeza NHIF kutafuta namna mbadala ya kuwezesha kufanikisha azma ya Serikali ya kuwahakikishia wakulima wanapatiwa matibatu bora na ya uhakika. Hiyo ikawalazimu NHIF kutafuta na kushawishi Asasi za kifedha kukwasisha mpango huo wa Serikali. Ushawishi huo ukawezesha kuipata TPB ambayo imekubali kukwasisha mpango wa majaribio wa Ushirika Afya,” anasema Majala.

Mkoani Mwanza Wadau watatu kwa maana ya NHIF, TPB na NCU (1984) Ltd wameingia kwenye Randama ambapo TPB watakwasisha urajisishwaji wa wanachama wa vyama vya msingi vya ushirika wa mazao matano ya kimkakati kwa kuwakopesha fedha zisizotozwa riba kwaajili ya kulipia gharama za kujiunga na Ushirika Afya kwa mwanachama wa chama cha ushirika mwenza wake na wategemezi wengine wanne. Mkopo huo utakuwa kati ya Sh. 355,200/- hadi Sh. 460,800/- kwa mwaka kutegemeana na aina ya wategemezi ambao mwanachama wa Ushirika Afya atawaunganisha pamoja naye kama ilivyoelezwa katika mchanganuo ufuatao: Endapo mwanachama ataamua kujisajili yeye, mwenza wake na wanawe wanne wenye umri wa chini ya miaka kumi na minane (18) atakopeshwa kiasi cha Sh. 355,200/-; na Endapo mwanachama ataamua kujisajili yeye, mwenza wake na wazazi wake na wa mwenza wake atakopeshwa kiasi cha Sh. 460,800/-.

Mpango huu wa majaribio wilayani Magu umelenga kuwaonyesha wakulima wa mazao ya kimkakati thamani ya bima ya afya kwa wale ambao watatokea kufikwa na maradhi katika kipindi cha mwaka mmoja ili wawe rejea kwa wakulima wengine na hivyo kuongeza hamasa na utayari wa wakulima kujiunga na kuchangia bima ya afya. Uhamasishaji ulifanyika kwenye vyama vya msingi kumi katika Wilaya ya Magu na kulenga kurajisi wanachama mia tano (500). Vyama hivyo ni Bugatu AMCOS Ltd, Busangi AMCOS Ltd, Ipililo AMCOS Ltd, Mahaha AMCOS Ltd, Ndagalu AMCOS Ltd, Ng’haya AMCOS Ltd, Nhobola AMCOS Ltd, Nsobu AMCOS Ltd, Kabila AMCOS Ltd na Mwamagoli AMCOS Ltd.

# MIFUMO YA KUWEZESHA UPATIKANJI WA FEDHA KWA VYAMA VYA USHIRIKA WA NYUMBA

Mifuko ya ujenzi wa Nyumba za gharama nafuu ni njia inayotumika sana katika Mataifa mengi Duniani kuwezesha Vyama vya Ushirika wa Nyumba kuwa na fedha kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba za gaharama nafuu.  Sehemu nyingine mfumo huu huitwa Mifuko ya Ushirikiano (Solidarity Funds).

## Uanzishaji wa Mifuko ya  Ujenzi wa Nyumba za Gharama Nafuu

Mifuko ya ujenzi wa gaharama nafuu inaanzishwa kupitia Vyama vya ushirika wa nyumba ambavyo vimeandikishwa kwa mujibu wa sheria ya Vyama vya Ushirika. Kwa ujumla Vyama vya Ushirika wa Nyumba hutumika katika nchi mbalimbali ili kuwezesha wananchi wa kipato cha chini na cha kati waweze kumiliki nyumba. Bidhaa zinazoweza kutolewa katika vyama hivi hutegemea zaidi mahitaji ya wanachama na jamii kwa ujumla, uwezo wa chama kifedha, hali ya uchumi unatoa fursa zinazowezesha chama kutoa huduma bora na kwa wakati kwa wanachama wake.



*Moja ya Nyumba za Ushirika wa nyumba Muungano, Chamazi – Dar es Salaam*

Bidhaa na huduma zinazoweza kutolewa na Vyama vya Ushirika wa Nyumba ni kama vile: kujenga nyumba za wanachama za kuishi; nyumba za kupangisha; kuwapa wanachama wake mikopo ya vifaa vya ujenzi kama vile saruji, mabati na mbao, ambapo wanachama wanaweza kuwa wanalipa kidogo kidogo kwa muda maalumu na kwa kufuata utaratibu waliojiwekea; kutoa mikopo ya kuwezesha wanachama wake kununua nyumba ambazo tayari zimekamilika; kusaidia wanachama kupata mikopo kwa ununuzi wa viwanja vya ujenzi wa nyumba; kutoa mikopo ya ukarabati wa nyumba; na kutoa mikopo ya ujenzi wa miundombinu ya nyumba kama vile kuweka umeme, maji na kuboresha mfumo wa maji taka. Ili chama kiweze kutoa huduma kwa ufanisi, inabidi kiweze kuwa na fedha za kutosha. Hivyo, mfumo mmojawapo ni kuwa na Mfuko wa ujenzi wa Nyumba za gharama nafuu.

## Lengo la Mifuko ya Ujenzi wa Nyumba za Gharama Nafuu

Lengo kuu la mifuko ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu ni kuwa na mfumo endelevu wa kifedha wenye kuhakikisha uwepo wa fedha na kuhamasisha uendelezaji wa nyumba za gharama nafuu kwa kwa wananchi wa kipato cha chini kupitia asasi ambazo zitaanzishwa na kusimamiwa na wananchi wenyewe. Asasi hizo ni Vyama vya ushirika wa nyumba au vyama vya ujenzi.

Mifuko ya Ujenzi wa Nyumba za Gharama Nafuu inayoweza kuanzishwa itakuwa na madhumuni yafuatavyo:

**a)** Kuwezesha wananchi ambao ni wanachama wa Vyama vya Ushirika wa Nyumba kuwa na fedha za kukidhi gharama za kukunua viwanja, kulipia gharama za upimaji na, umilikishwaji;

**b)** Kuwezesha upatikanaji wa fedha na kuwezesha utoaji wa mikopo ya nyumba kwa wanachama kwa ajili ya nyumba za makazi;

**c)** Kuwezesha upatikanaji wa ardhi, vifaa na zana za ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa kununua vifaa vya ujenzi kwa pamoja ili kupunguza gharama za ujenzi;

**d)** Kuwezesha Vyama vya Ushirika wa Nyumba kuwa na dhamana zenye kuwezesha Vyama hivyo kukopesheka ili kupata mikopo ya nyumba kutoka kwenye taasisi za fedha; na

**e)** Kufanya shughuli nyingine zote kama itakavyoidhinishwa katika madhumuni ya miongozo ya uendeshaji wa mifuko hiyo au masharti ya Vyama vya Ushirika wa Nyumba.

## Vyanzo vya Fedha za Mifuko ya Ujenzi wa Nyumba

Vyanzo vya fedha za Mifuko ya Ujenzi wa Nyumba za Gharama Nafuu zitatokana na Akiba za wanachama katika mifuko, ambapo Vyama vyenyewe kupitia mikutano mikuu vitaweka utaratibu wa kiasi cha akiba ambayo itatakiwa kuchangiwa na wanachama katika mifuko hiyo kwa kila mwezi au muda wowote kwa kadri itakavyopangwa. Vyanzo vingine vya fedha za Mifuko ni Mikopo na misaada mbalimbali; na Ziada itakayopatikana na kuidhinishwa iweze kuingizwa kwenye mifuko kwa idhini ya Mikutano mikuu.

Usimamizi wa Mifuko

Bodi za Uongozi zitakuwa ndivyo vyombo vya usimamizi wa mifuko hiyo na ikiwezekana zinaweza kukasimu madaraka yake kwa kamati maalum za uendeshaji wa mifuko hiyo kama ikionekana kuna haja ya kufanya hivyo.

Uendeshaji wa Mifuko

Ili kuleta ufanisi katika uendeshaji wa mifuko ya ujenzi wa nyumba za gaharama nafuu, kila chama cha Ushirika wa Nyumba kitatakiwa kutayarisha Mwongozo wa uendeshaji wa mfuko, ambapo pamoja na mambo mengine mambo yafuatayo yataainishwa:

- **i.** Sifa za wajumbe wa mifuko;
- **ii.** Majukumu ya Kamati za Usimamizi wa Mifuko;
- **iii.** Taratibu za uendeshaji wa Akaunti maalum za mifuko;
- **iv.** Taratibu za uwekaji wa akiba kwa ajaili ya ujenzi wa myumba;
- **v.** Taratibu za uombaji wa mikopo, upitishaji na utoaji wa mikopo. Hii ni pamoja na masuala ya mikataba ya mikopo na utoaji wa fedha kwa wanachama;
- **vi.** Dhamana za mikopo inayotolewa;
- **vii.** Ufuatiliaji wa shughuli za nyumba zinazoombewa mikopo;
- **viii.** Tengo la mikopo mibaya;
- **ix.** Hesabu za mifuko na taratibu za ukaguzi wa hesabu za fedha;
- **x.** Utoaji wa taarifa za mwaka za maendeleo ya mifuko; na
- **xi.** Mipaka ya mifuko.Mwandishi wa makala hii ni Bw. Bahati J. Rukiko, Afisa Programu Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU).

# TARATIBU ZA UINGIAJI WA MIKATABA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

Kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002, Ushirika ni muungano wa watu waliojiunga pamoja kwa hiari kwa madhumuni ya kufanikisha mahitaji yao, kwa kuanzisha na kumiliki chombo chao kidemokrasia na kuchangia mtaji unaohitajika kwa usawa na kukubali kuyakabili matatizo na kupata manufaa kutokana na shughuli zao ambazo hushiriki kikamilifu.

Kifungu cha 35 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 kinaeleza kuwa Chama cha Ushirika ni taasisi yenye hadhi ya Kisheria (Legal Entity) ambayo inaweza kuingia mikataba, kushtaki au kushtakiwa kwa mujibu wa Sheria. Kimsingi Vyama vya Ushirika vinapaswa kufuata taratibu za uingiwaji wa mikataba kama zilivyoainishwa katika Sheria mbalimbali za nchi ikiwemo Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 na Kanuni zake za Mwaka 2015, Sheria ya Mikataba sura ya 345 ya Mwaka 2002, Masharti ya Chama pamoja na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Ofisi ya Mrajis kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika.

Mikataba inayoingiwa na Vyama vya Ushirika

Pamoja na ukweli kwamba kuna aina nyingi za mikataba inayoingiwa na Vyama vya Ushirika kuna aina tatu za mikataba huingiwa zaidi na Vyama vya Ushirika, aina hizo ni: (i) Mikataba ya Bidhaa (Goods) inayohusisha zaidi ununuzi wa Pembejeo kama vile Mbolea, Madawa na Vifungashio; (ii) Mikataba ya Huduma (Services) hususan huduma za Mafunzo, Elimu,TEHAMA na Ukusanyaji Madeni; na (iii) Mikataba ya ujenzi na ukarabati wa majengo ikiwemo Maghala na Ofisi za Vyama vya Ushirika.

Kwa kuzingatia aina tatwa hapo juu, taratibu za uingiwaji wa mikataba katika Vyama vya Ushirika zimegawanyika katika makundi makuu mawili kama ifuatavyo;

## (i)Taratibu za Kiushirika

Taratibu hizi zinazingatia Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika, Masharti ya Vyama pamoja na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Ofisi ya Mrajis. Taratibu hizi zinaelekeza pamoja na mambo mengine kwamba; ili Chama kiingie Mkataba ni lazima kwanza kipate idhini ya Wanachama wake kupitia Mkutano Mkuu. Baada ya kupata ridhaa ya Mkutano Mkuu, Chama ninapaswa kuwasilisha rasimu na nyaraka za mkataba husika katika Ofisi ya Mrajis kwa ajili ya kupitiwa (vetting) na kupata kibali cha kuingia mkataba tajwa. Nyaraka za mkataba zinazohitajika kwa ajili ya kupitiwa ni pamoja na rasimu ya mkataba wenyewe, Muhtasari wa Mkutano Mkuu na kikao cha Bodi husika na nyaraka za mchakato wa zabuni kama uliofanyika.

Aidha taratibu hizo zinaelekeza mikataba yenye thamani ya chini ya kiasi cha shilingi milioni mia tano (500,000,000) itapitiwa na kupewa kibali katika ngazi ya Mrajis Msaidizi wa Mkoa husika na mikataba inayozidi kiasi cha shilingi milioni mia tano (500,000,000) itapitiwa na kupewa kibali katika ngazi ya Mrajis Taifa.

## (ii) Taratibu za Kimkataba

Ili mkataba uweze kukamilika ni lazima taratibu za Sheria ya Mkataba (The Law of Contract Act) sura ya 345 (2002) zizingatiwe pia, taratibu hizo ni pamoja na kuwepo kwa Makubaliano (Agreement) na masharti ya makubaliano (Terms and Conditions) kulingana na aina ya mkataba husika. Aidha ni lazima pia Chama cha Ushirika kiwe na uwezo Kisheria wa kuingia mkataba husika kwa mujibu wa sheria za nchi kulingana na aina ya mkataba.

## Hitimisho.

Pamoja na kuanishwa kwa taratibu tajwa hapo juu Vyama vingi vinaingia mikataba bila kufuata taratibu za Kiushirika na zile za kimkataba hali inayopelekea migogoro mingi ya Kisheria ikiwemo kesi Mahakamani na hata kusababisha hasara kwa Vyama. Hivyo basi Vyama vyote vya Ushirika pamoja na Wadau wanaoingia mikataba na Vyama hivyo wanapaswa kuzingatia taratibu zilizoainishwa ili kuepuka migorogoro na kuwa na mikataba yenye tija kwa Maslahi ya Vyama, Wanachama na Wadau kwa ujumla.

# VIONGOZI WA USHIRIKA MKOANI KAGERA WAPEWA MAFUNZO

Elimu kwa Wakulima imeelezwa kuwa ni njia ya kuleta chachu kwa Ushirika hapa nchini ili kuwainua na kufikia lengo lililokusudiwa.

Akifunga mafunzo kwa Viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika kutoka Wilaya za Kyerwa na Karagwe yaliyoandaliwa na Chama Kikuu cha Ushirika Karagwe na Kyerwa KDCU LTD kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi, Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mh. Brigedia Michael Gaguti amewataka washiriki wa mafunzo hayo kuzingatia na kuitumia elimu waliyoipata kuhakikisha inaleta tija na kuondoa kero kwa wakulima.

Aidha mkuu huyo wa mkoa wa Kagera alitumia fursa hiyo kuwapongeza Viongozi wa vyama Vikuu mkoani humo (KDCU LTD na KCU) Kwa kufanya kazi vizuri ya ukusanyaji wa Kahawa kwa msimu wa mwaka 2020/21 na kuongeza kuwa ndani ya miaka mitatu ukusanyaji wa kahawa umetoka tani elfu Hamsini (50,000) hadi kufikia tani elfu sabini na nne (74,000) lengo ikiwa nikukusanya tani laki moja za maganda.

Mhe. Michael Gaguti ametoa onyo kwa mtu au kundi la watu ambao wamekuwa na fikira za kutaka kuvuruga na kusambaratisha Ushirika katika mkoa wa Kagera kuwa atachukuliwa hatua kali na vyombo vya dola. “nasisitiza kuwa kama kuna watu wana mawazo hayo, ni bora watafute kazi nyingine za kufanya au wajiunge na Ushirika.

Mkuu huyo wa Mkoa alionesha masikitiko yake hasa pale kila msimu wa kahawa unapokaribia kuanza kunapojitokeza watu wenye lengo la kuhujumu juhudi za serikali katika kuhakikisha Ushirika unasimama na kuwaletea wakulima maendeleo na hasa kupitia kilimo cha Kahawa,” alisema Mkuu wa Mkoa

Sanjari na hayo Mhe. Michael Gaguti amezindua na kugawa Pikipiki 18 kwa maafisa Ugani zilizotolewa na Chama Kikuu Cha Ushirika Karagwe na Kyerwa (KDCU LTD). Akitoa taarifa kwa mgeni rasmi Meneja Mkuu wa Chama hicho cha(KDCU LTD) Bw. Oscar Dominick amesema kuwa lengo kubwa ni kumfikiwa mkulima wa Kahawa ili kuboresha na kuhamasisha kilimo chenye tija na kufikia lengo la ukusanyaji wa tani laki moja za Kahawa ya maganda mkoani humo.



*Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mhe. Brigedia Michael Gaguti akikabidhi Pikipiki 18 kwa maafisa Ugani zilizotolewa na Chama Kikuu Cha Ushirika Karagwe na Kyerwa (KDCU LTD) Mkoani Kagera*

# MASWALI NA MAJIBU KUHUSU MIKUTANO MIKUU YA WANACHAMA WA VYAMA VYA USHIRIKA

## 1. Zipi ni ngazi za maamuzi katika vyama vya ushirika?

I.) Menejimenti
II.) Kamati
III.) Bodi
IV.) Mkutano Mkuu

## 2. Je, nini umuhimu wa mikutano mikuu katika vyama vya ushirika?

Mikutano Mikuu ya Wanachama katika Vyama vya Ushirika ndio yenye Mamlaka ya mwisho kwenye Chama cha Ushirika. Hivyo, maamuzi makuu yote yanayohusu uendeshaji na usimamizi wa Chama cha Ushirika hufanyika kwenye Mikutano Mikuu.

3. Kuna aina zipi za Mikutano Mikuu katika Vyama vya Ushirika?
I.) Mkutano Mkuu wa mwaka
II.) Mkutano Mkuu wa kawaida
III.) Mkutano Maalum

## 4. Nani anapaswa kushiriki Mikutano Mikuu ya Ushirika?

I.) Kwenye Chama cha Msingi Wajumbe ni wanachama wote ila Sheria inaruhusu kwa Vyama vyenye Wanachama wengi kuwa na mikutano ya uwakilishi.
II.) Kwenye Vyama Vikuu wajumbe wawakilishi kutoka kwenye vyama wanachama.
III.) Wanufaika wa Chama cha Ushirika (mfano wakulima) wanaweza kuhudhuria kwenye Mkutano Mkuu lakini hawaruhusiwi kushiriki, kuchangia wala kutoa maamuzi katika Mikutano.

## 5. Agenda za Mikutano Mikuu ni zipi?

Baadhi ya agenda zinazojadiliwa kwenye mikutano mikuu ni pamoja na:
I.) Kuchagua, kusimamisha au kufukuza wajumbe wa Bodi
II.) Kupokea taarifa ya ukaguzi mahesabu ya Chama
III.) Kuidhinisha mgao wa faida kwa Wanachama
IV.) Kuidhinisha kiwango cha Honoraria kwa Wajumbe wa Bodi na Watumishi wa kujitolea
V.) Kupokea na kujadili Taarifa ya Bodi
VI.) Kuidhinisha ununuzi au uuzaji wa mali za Chama kwa kuzingatia masharti ya Chama husika
VII.) Kupokea au kufukuza wanachama
VIII.) Kupitisha bajeti ya mapato, matumizi na ukomo wa madeni
IX.) Kupitisha marekebisho ya masharti, kupitisha Sera, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Chama
X.) Kuteua mkaguzi wa nje

# USHIRIKA UNAJENGWA NA VIONGOZI WALIO TAYARI KUJITOLEA

Viongozi wa Vyama vya Ushirika nchini wametakiwa kuwa tayari kujitolea na kuacha kuingia kwenye uongozi kwa kuangalia maslahi yao binafsi na badala yake wanahitajika viongozi waadilifu na wenye maono ya kusimamia mali za wanachama kwa maendeleo ya wote.

Wito huo umetolewa na Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini, Charles Malunde, kwenye Mkutano Mkuu wa 17 wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo KAWOSA Ltd (Karagwe Women SACCOS) uliofanyika Novemba 11, 2020 Mjini Kayanga, Karagwe – Kagera.

"Ushirika unajengwa na Viongozi walio tayari kujitolea hivyo kama kuna kiongozi anayeonekana kuingia kwa kuangalia maslahi yake binafsi hafai kuchaguliwa kuingia katika Viongozi wapya wanaowahitajika sasa," amesema Naibu Mrajis.



*Naibu Mrajis Charles Malunde akieleza jambo wakati wa Mkutano Mkuu wa Wanachama wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo KAWOSA Ltd (Karagwe Women SACCOS)*

Bw. Malunde amezitaka Kamati za Usaili ambazo zinashirikisha vyombo vya Usalama, kuhakikisha kuwa Wagombea watakaoletwa kwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu kupigiwa kura wawe wanaojulikana kwa uadilifu na uaminifu ili kuvifanya vyama viendele mbele.

"Viongozi watakaochaguliwa wanapaswa kufahamu kuwa wamepewa dhamana na wanachama wenzao katika kuendesha chama chao. Hivyo, wanapaswa kuhakikisha kuwa chama kinaendeshwa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Masharti ya Chama," amesema Naibu Mrajis.

Viongozi wanapaswa wafahamu kuwa mwanachama anahitaji kuona matunda ya ushirika wake na si vinginevyo na kwamba chama cha ushirika si sehemu ya kwenda kuchuma mali na kisha kuondoka, kikiachwa chama kikiwa hoi. Tabia hii ya kizamani na isiyofaa haina nafasi tena katika Serikali hii ya Awamu ya Tano.

Aidha, wanachama wanapaswa kufahamu kuwa iwapo wataona mambo hayaendi vizuri wana nafasi ya kuitisha Mkutano Mkuu Maalum kwa mujibu wa Masharti ya chama chao na kuchukua hatua ya kuiondoa Bodi kama itaenda kinyume na Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba 6 ya Mwaka 2013 na Kanuni zake za 2015, Masharti na Sera za Chama chao.

"Imejengeka mazoea, inapofikia wakati Vyama vya Ushirika vinaposhindwa kufanya vizuri lawama zinaelekezwa kwa Serikali wakati wasimamizi nambari moja ni wanachama wenyewe. Hili linapaswa lizingatiwe ili kuweza kuepuka migogoro isiyokuwa na maana katika Vyama vya Ushirika," amesema Bw. Malunde.

Aidha, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Kagera, Godfrey Mpepo, amewataka Viongozi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Kagera watakaochaguliwa kuwa waadilifu na wenye uwezo wa kusimamia mali na rasilimali za Vyama vyao kwa kujali maslahi ya Wanachama na Jamii kwa ujumla.
"Baada ya kuchaguliwa viongozi wa Ushirika wanatakiwa kuweka malengo ya muda mfupi na mrefu watakayotekeleza ili kuleta tija kwenye Vyama. Malengo hayo ni pamoja na kuhakikisha kwamba uandishi na utunzaji wa hesabu za vyama unapewa kipaumbele ili kuwezesha upatikanaji wa Hati Safi wa taarifa za ukaguzi wa COASCO," amesema Mpepo.

Viongozi wa Ushirika wameaswa kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha za chama kwa mujibu wa bajeti zao zilizopitishwa na Wanachama kwenye Mikutano na kuidhinishwa na Mrajis kwa lengo la kujenga Vyama imara na vyenye nguvu vinavyojitegemea kiuchumi.

Akisoma Taarifa yake kwenye Mkutano Mkuu, Mwenyekiti wa KAWOSA, Safina Mrisho, amesema chama hicho kimepata mafanikio makubwa tangu kianzishwe ambapo chama kilianza na Wanachama 70 na baada ya miaka 14, kuna Wanachama sasa 3,587; Akiba za Wanachama zimeongezeka kutoka Shilingi 3,133,000 mwaka 2006 hadi Shilingi 717,359,230 mwaka 2020; Kwa mwaka 2006 hisa zilikuwa Shilingi 696,000 na kwa sasa ni Shilingi 293,363,395; na Amana kwa Mwaka 2006Wanachama walikuwa hawaweki na sasa kuna amana Shilingi 119,425,263.



*Baadhi ya Wanachama wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo KAWOSA Ltd (Karagwe Women SACCOS)*



Meneja wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo KAWOSA Ltd (Karagwe Women SACCOS) Golieth Elias akisoma taarifa ya Chama hicho wakati wa Mkutano Mkuu wa Wanachama

# MADIWANI WAPIGWA MSASA DHANA YA USHIRIKA



Ofisi ya Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Iringa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) tawi la Iringa wametoa Mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani wa Wilaya ya Mufindi kuhusu Dhana ya Ushirika. Mafunzo yaliyofanyika wakati wa Semina elekezi kwa Waheshimiwa Madiwani wa Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa.

"Ushirika tumepata fursa ya kutoa Elimu juu ya Dhana ya Ushirika kwenye semina zinaendelea za Waheshimiwa Madiwani na kesho tutakuwa Wilaya ya Iringa Vijijini na Manispaa," amesema Robert George, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Iringa. Katika hatua nyingine mkoani Ruvuma kumetolewa Mafunzo ya Dhana ya Ushirika na Majukumu ya Waheshimiwa Madiwani katika kuimarisha Ushirika katika mkoa huo. Mafunzo yaliyofanyika kupitia Mikutano ya Mabaraza ya Kuapisha Madiwani inayoendelea katika Halmashauri nane (8) za mkoa wa Ruvuma.

Mafunzo yanatolewa na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Ruvuma, Bumi Masuba na Mkufunzi kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi tawi la Ruvuma, Evaristo Mwamhanga.

Miongoni mwa masuala yaliyoelekezwa katika mafunzo hayo ni pamoja na Misingi ya Ushirika Kimataifa ikiwemo Uanachama wa hiari, demokrasia, Ushiriki wa wanachama katika shughuli za Kiuchumi, Uhuru na kujitegemea na Elimu, mafunzo na taarifa, Ushirikiano miongoni mwa Vyama vya Ushirika pamoja na kuijali Jamii.



*Madiwani wapya waliochaguliwa baada ya uchaguzi Mkuu wakiwa katika Mafunzo ya Ushirika Mkoani Ruvuma*

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA KILIMO
# TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

Anuani ya Simu: "Ushirika"
Simu: +255 26- 23 22456
Telefax: +255 26 - 23 21973
B.Pepe: ushirika@ushirika.go.tz
Tovuti: www.ushirika.go.tz

Mtaa wa Kuu,
S.L.P. 201,
DODOMA.

## TAARIFA KWA UMMA

## VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO (SACCOS) VYATAKIWA KUFUNGA HESABU KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA DESEMBA 31, 2020

Mwaka wa Fedha wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) unaanzia Mwezi Januari na kuisha Mwezi Desemba kila mwaka. Mara baada ya kupita kwa muda huo, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amezitaka SACCOS zote kuhakikisha zinafunga Hesabu zake za Mwaka husika kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 55(2) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 na kanuni ya 55 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015 na kutakiwa kuziwasilisha kwa Mkaguzi wa Nje (Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika - COASCO).

Katika kutekeleza matakwa haya ya Sheria na Kanuni, Mrajis amewaelekeza Viongozi wa SACCOS nchini kuhakikisha wanafunga Hesabu za Mwaka 2020 mapema na kuziwasilisha kwa Wakaguzi wa Nje ndani ya Mwezi wa Januari 2021, ili hesabu hizo ziweze kukaguliwa na kurudishwa kwao mapema.

Viongozi wa SACCOS wanapaswa kujibu hoja zote zilizotolewa na zitakazotolewa na Wakaguzi ili kuondokana na uwepo wa Hati Zisizoridhisha pamoja na Hati Chafu. Chama kitakachoshindwa kujibu hoja husika na kupata Hati Chafu, Viongozi na Watendaji wake watapaswa kuwajibika kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 55(13) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika, kanuni ya 85(g) ya Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) za Mwaka 2019.

Ofisi ya Mrajis katika ngazi ya Taifa na katika mikoa yote itafuatilia utekelezaji wa maelekezo haya kwa karibu na kuchukua hatua stahiki kwa wote watakaobainika kwenda kinyume na maelekezo haya na kushindwa kutekeleza matakwa ya Sheria na Kanuni zake kama zinavyoelekeza.

Aidha, Mrajis amewakumbusha na kuwahimiza viongozi wa SACCOS nchini kuhakikisha wanaomba Leseni kwa wakati ili kuepuka usumbufu na adhabu zinazoweza kutolewa kwao iwapo watashindwa kuomba na kupata leseni kwa wakati katika kipindi cha mpito kilichotolewa na Serilikali. Hesabu zilizokaguliwa na Mkaguzi wa Nje zinatakiwa kutumika katika zoezi la kuomba Leseni kwa SACCOS, ambazo hazijaomba leseni hadi kufikia tarehe ya Taarifa hii.

# ELIMU YA USHIRIKA IWAFIKIE WANACHAMA WOTE - NAIBU MRAJIS

Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika Nchini, Collins Nyakunga ametoa wito kwa Vyama vya Ushirika kuhakikisha kuwa vinatoa elimu ya Ushirika kwa Wanachama wao kwa Mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013.



*Naibu Mrajis Collins Nyakunga akitoa Salamu za Ushirika wakati wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika, Jijini Dodoma*

Wito huo umetolewa wakati akifungua mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi mbalimbali za Vyama vya Ushirika wanachama na Wadau wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika nchini (TFC) Desemba 10, 2020 Jijini Dodoma.

Naibu Mrajis amesema ni muhimu elimu ya Ushirika kuwafikia Wanachama wa Vyama vya Ushirika ili kuwawezesha kuwa na uelewa mpana wa masuala yanayofanyika katika Vyama vyao. Hivyo amewataka viongozi wa Ushirika waliokuwa katika mafunzo hayo kuhakikisha mambo muhimu watakayojifunza katika mafunzo hayo wanayafikisha kwa wanachama wao.

"Viongozi mna wajibu wa kuwaandaa wengine kuwa Viongozi kwa kuhakikisha kuwa Wanachama wenu wanapata elimu ya Ushirika; elimu ya Ushirika si ya viongozi tu bali ni kwaajili ya Wanachama wote kwakuwa hii ni haki yao ya Msingi ya Kiushirika," alisisitiza Naibu Mrajis

Aidha, Bw. Nyakunga ametumia fursa hiyo kuwakumbusha Viongozi wa Ushirika kuendelea kutenga Fedha kutoka kwenye mapato ya ndani ya Vyama kwaajili ya kutoa elimu kwa Wanachama, Wajumbe wa Bodi, Viongozi na Watendaji kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika.

Baadhi ya Masuala muhimu yaliyoko katika mafunzo hayo ni pamoja na kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika, Dhana ya Ushirika, Utawala Bora, Wajibu wa Viongozi wa Vyama vya Ushirika, elimu ya Biashara, masuala ya Rushwa pamoja na mengine yatakayoongeza tija na ufanisi kwenye Vyama.
Akizungumza katika mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Shirikisho, Theresia Chitumbi amesema Mafunzo hayo yamelenga kuongeza uelewa wa Ushirika kwa Wanaushirika na ametoa rai kwa Vyama vya Ushirika kuendelea kujiunga na Shirikisho hilo ili kuwa na Sauti ya pamoja katika Vyama vya Ushirika.
Akieleza mikakati inayoendelea kutekelezwa na Shirikisho hilo Chitumbi ameeleza kuwa Shirikisho liko katika jitihada za kuunga mkono juhudi za Serikali za kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Viwanda. Ambapo Shirikisho lipo katika hatua za awali za mikakati ya kuanzisha Kiwanda cha Vifungashio vya Magunia pamoja na Kiwanda cha Mbolea.

Mwenyekiti wa TFC amesema kuwa Mafunzo hayo yatafuatiwa na Mkutano Mkuu wa 25 wa Shirikisho hilo uliofanyika Desemba 11, 2020 Jijini Dodoma. Mkutano uliojumuisha Wajumbe, Viongozi, Wanachama na Wadau mbalimbali wa Ushirika kwaajili ya kujadili masuala na taarifa mbalimbali za Shirikisho hilo ili kupanga mikakati na mipango ya mbele ya Shirikisho hilo.

# ELIMU YA FEDHA KUIMARISHA USHIRIKA NCHINI

Elimu ya Fedha imetajwa kuwa moja ya nyenzo muhimu katika kuimarisha na kuendeleza Ushirika kwa lengo la kuunga mkono jitihada za Serikali za kuondoa umaskini na kuinua uchumi wa Wananchi.
Hayo yamesemwa na Mgeni rasmi Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera Prof. Faustine Kamuzora wakati wa Sherehe zilizofanyika Bukoba Mkoani Kagera kukabidhi Vyeti kwa Wahitimu wa Programu za mafunzo ya Uongozi na Usimamizi pamoja na Utunzaji wa Hesabu za Vyama vya Ushirika kwa njia ya masafa. Mafunzo yaliyokuwa yakitolewa na kuratibiwa na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) kwa viongozi wa Vyama vya Ushirika wa mikoa ya Kagera, Tabora, Geita na Simiyu.



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera Prof. Faustine Kamuzora akikabidhi Cheti kwa mhitimu mafunzo ya Ushirika, Zaituni Dotto. Katikati ni Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege akifuatiwa na Mrajis Msaidizi wa Mkoa wa Kagera, Godfrey Mpepo*

Akiongea katika Sherehe hizo Prof. Kamuzora amewataka Wahitimu hao ambao wengi wao ni Viongozi wa Vyama vya Ushirika kutumia elimu waliyopata katika kusimamia Vyama vya Ushirika kwa weledi ili kulinda maslahi ya Wanachama wa Ushirika. Akisisitiza suala la Viongozi hao kutumia elimu ya fedha waliyopata kuongeza na kubuni mbinu mbalimbali za kuongeza vipato kwa Vyama vyao vya Ushirika wanavyosimamia.

“Hakikisheni mnaendelea kuitumia elimu ya Fedha mliyoipata kwaajili ya kuimarisha na kuongeza mapato ya Vyama vya Ushirika na elimu hiyo mkawashirikishe Wanachama katika Vyama vyenu vya Ushirika” alisema Prof. Kamuzora
Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege katika hotuba yake amewataka Viongozi waliopata mafunzo ya Ushirika kwenda kuleta mabadiliko chanya katika Vyama wanavyosimamia, akisisitiza utendaji utakaondoa changamoto za ubadhilifu na Hati zisizoridhisha ambazo zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara.

“Moja ya sababu ambazo zimekuwa zikileta changamoto katika Sekta ya Ushirika ni watendaji na Viongozi kutokuwa na uelewa sahihi wa namna bora ya utunzaji wa hesabu na Kumbukumbu za Vyama vya Ushirika, ni imani yangu mafunzo haya yanakwenda kuongeza ufanisi na Hati safi kwa Vyama vyetu,” alisema Mrajis

Aidha, Mrajis ametoa wito kwa Wanawake wengi kushiriki nafasi mbalimbali za Uongozi wa Vyama vya Ushirika hususani wakati huu ambao Vyama vingi vya Ushirika vinakwenda kufanya Uchaguzi wa nafasi za Uongozi ikiwemo Wajumbe wa Bodi, Mameneja na Watendaji wengine.

Mrajis Ndiege pia aliwataka Warajis Wasaidizi wa Mikoa kwa kushirikiana na Maafisa Ushirika wa Wilaya katika Mikoa mingine kuendelea na jitihada za kujiendeleza kimaarifa hususani katika masuala ya Uandishi mzuri wa Vitabu vya Ushirika mara baada ya msimu wa mazao ili kuondokana na dosari mbalimbali zinazoleta taswira hasi kwa Sekta ya Ushirika.

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU) Prof. Alfred Sife alieleza kuwa mafunzo hayo awali yalikuwa yakifanyika kwa njia ya Posta, ambapo hivi sasa kutokana na maendeleo ya kiteknolojia mafunzo ya Ushirika yanafanyika kwa masafa. Mkuu huyo alifafanua kuwa utoaji huo wa elimu ni miongoni mwa mikakati ya Chuo hicho katika kuhakikisha wigo wa upatikanaji wa elimu unaongezeka na Vyama vya Ushirika vinakuwa imara zaidi kwa kuwafikishia mafunzo mahali walipo.

Baadhi ya masuala yaliyotajwa kuwa ni sehemu ya mafunzo hayo ni pamoja uelewa wa dhana ya Ushirika, Misingi ya Ushirika, Uongozi wa Asasi za Ushirika, Kanuni za Utunzaji wa Mahesabu ya Ushirika, uchanganuzi wa Ushirika wa mazao, utunzaji Kumbukumbu pamoja na mada nyingine zenye kuongeza tija ya utendaji wa Vyama vya Ushirika.

Katika Sherehe hiyo jumla ya Viongozi 120 wamehitimu mafunzo hayo ya Ushirika na kukabidhiwa Vyeti vya kumaliza mafunzo. Akisoma risala kwa niaba ya Wahitimu Mjumbe wa Bodi KDCU Bw. Fidolin Kasenene ameshukuru Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi pamoja na Wadau wa Ushirika waliofanikisha mafunzo hayo, huku akiomba mafunzo kama hayo yawe endelevu ili kuongeza ufanisi na usimamizi bora wa Vyama vya Ushirika nchini.



*Baadhi ya Wahitimu wa Mafunzo ya Ushirika ya Uongozi na Usimamizi pamoja na Utunzaji wa Hesabu za Vyama vya Ushirika kwa njia ya masafa mara baada ya kupokea Vyeti vyao*

# TANESCO SACCOS KUJENGA JENGO LA OFISI

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo TANESCO kimeanza mchakato wa shughuli za ujenzi wa jengo la ofisi baada ya kukamilika kwa taratibu za kuhamisha hati ya kiwanja kutoka Chama cha Ushirika wa Nyumba Mwenge (MHCS) kuja TANESCO SACCOS. Akisoma Taarifa yake kwenye Mkutano Mkuu uliofanyika kwa siku mbili tarehe 14 - 15 Novemba, 2020 Jijini Dar Es Salaam, Mwenyekiti wa TANESCO SACCOS, Somoe Nguhwe amesema chama kimempata Mshauri Mwelekezi wa mradi wa ujenzi (Consultant) ambaye ameanza kazi kwa kuandaa michoro na kuandaa nyaraka za kumpata mjenzi (Contractor).



*Baadhi ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Ushirika TANESCO SACCOS wakifuatilia mada mbalimbali zilizofanyika Jijini Dar es Salaam*

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, amewapongeza viongozi wa TANESCO SACCOS kwa hatua ya kuanza taratibu za ujenzi wa jengo la ofisi.

"Nichukue nafasi hii kuwasihi viongozi kuendelea na mchakato wa utekelezaji wa mradi huo wa ujenzi aa jengo la ofisi, ili kukuza taswira ya Chama na kuokoa gharama zinazoingiwa na Chama kulipa kodi ya pango," amesema Dkt. Ndiege. Hata hivyo, Dkt. Ndiege amesema kuwa ujenzi huo lazima uzingatie maslahi ya wanachama na kutowafanya wanachama kukosa mikopo kwa kisingizio cha kujenga. Pia ujenzi huo ufuate kikamilifu sheria na miongozo ya manunuzi na uwekezaji kwenye vyama vya ushirika.

Mrajis amekipongeza Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo TANESCO kwa kuwa kati ya vyama vichache vilivyoweza kupata Hati Safi na kudhihirisha kuwa chama hicho kimeendelea kusimamia mali za wanachama kwa uaminifu. Dkt. Ndiege amewapongeza viongozi na wanachama wa TANESCO SACCOS kwa hatua madhubuti wanayoichukua ya uwekezaji katika taasisi za ndani ya Sekta kwa maana uwekezaji katika ya Benki wa Ushirika (KCBL).

"Niwahakikishie kwamba serikali kupitia Benki Kuu (BoT) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) imejipanga kusimamia benki hii muhimu kwa wanaushirika na watanzania kwa ujumla. Niwahakikishie hii ni fursa muhimu sana ya uwekezaji," amesema Dkt. Ndiege.

Mkutano Mkuu wa TANESCO SACCOS kwa mwaka huu ni wa uchaguzi ambapo Wajumbe watachagua viongozi ambao watasimamia Chama kwa kipindi cha miaka mitatu. Dkt. Ndiege amewaasa wajumbe wa Mkutano Mkuu kuwa makini kuhakikisha kuwa wanachagua viongozi mahiri ambao wataendeleza kazi nzuri iliyofanywa na Uongozi unaomaliza muda wao.

"Uongozi wa Chama ndiyo Dira kwa maendeleo ya Chama kwani kama uongozi ukiwa legelege uwezekano wa kuua Chama ni mkubwa kwani wanachama watakosa imani. Hivyo kabla ya kuchagua hakikisha unatafakari usichague kwa ushabiki," amesema Mrajis.

Kwa kuzingatia utendaji mzuri wa Bodi iliyo maliza kazi yake, na Kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013, Kifungu cha 137 kinampa Mrajis mamlaka ya kuteua mjumbe / wajumbe wa Bodi ambao ataona wanafaa kushika nafasi ya ujumbe huo kwa maslahi ya umma na chama kwa ujumla.

Kwa kuzingatia mamlaka haya aliyonayo Mrajis, amemteua Bi. Somoe Nguhwe ambaye atakuwa sehemu ya Bodi ya TANESCO SACCOS kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi, ubora wa huduma pamoja na kuendelea kuimarisha Sekta ya Ushirika wa Akiba na Mikopo nchini na nje ya nchi. Aidha, Lengo kubwa ni kuendeleza ushirikiano kwenye taasisi zetu za Ushirika nchini (SCCULT) pamoja na ushirikiano wa nje ya nchi (ACCOSCA na WOCCU).

Bi. Somoe Nguhwe amekuwa mwanachama mwenye uzoefu mkubwa na amesomea na kufanya kazi za masuala ya ushirika kwa kipindi kirefu tangu Mwaka 1984. Mwanachama huyu amekuwa na uzoefu kwenye nafasi ya uongozi na utendaji kazi kwenye SACCOS tangu Mwaka 1981.

Dkt. Ndiege amesema kuwa Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania imedhamiria kuimarisha utendaji kazi wa Vyama vya Ushirika nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea kuweka taswira nzuri ya Ushirika kwa umma ili wananchi wengi waweze kuvutiwa na kuendelea kutumia huduma na bidhaa zinazotolewa na Vyama vya Ushirika nchini.

# WANAWAKE WAHAMASISHWA NAFASI ZA UONGOZI WA USHIRIKA

Wito umetolewa kwa Wanawake kushiriki katika nafasi za uongozi katika Vyama vya Ushirika hususani Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) nchini pindi nafasi hizo zinapojitokeza.
Wito huo umetolewa na Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini, Charles Malunde alipokuwa akifungua Kongamano la Wanawake kuelekea maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo. Maadhimisho Oktoba 12, 2020 na kilele chake kilichokuwa Oktoba 15, 2020 Jijini Arusha.

Naibu Mrajis amesema Ushirika nchini umekuwa chachu ya maendeleo katika kuhakikisha kuwa makundi ya watu wa kipato cha chini na maskini katika jamii wanakuwa na chombo cha kuaminika cha kuwawezesha kufikia malengo yao ya kiuchumi na kijamii.

Aliongeza kuwa licha ya ushirika nchini kuendelea kushamiri katika sekta mbalimbali za kiuchumi na Vyama kujiendesha kwa kufuata Misingi ya Ushirika kimataifa bado kuna changamoto katika sekta ya Ushirika katika masuala yanayohusu jinsia na nafasi ya mwanamke katika uongozi wa vyama vya Ushirika.

"Ushiriki wa wanawake katika sekta ya Ushirika umekuwa kidogo sana hivyo hali hii ikiendelea kuwa hivi itapelekea kutokuwa na uendelevu katika shughuli za kiushirika katika miaka ijayo. Kukosekana kwa chombo cha kitaifa cha kuwaunganisha wanawake katika sekta ya Ushirika kunapelekea kukosa uwakilishi katika anga za kimataifa na kukosa fursa za kimaendeleo," alisema Naibu Mrajis

Akifafanua suala la nafasi ya uongozi kwa wanawake Naibu huyo alisema katika kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika shughuli za ushirika nchini.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na wadau wengine itahakikisha kuwa uhamasishaji unaendelea kunafanyika ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika Vyama vya Ushirika vikiwepo Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo kwa kuwatengenezea mazingira rafiki ikiwemo kuwa na chombo cha kitaifa kitakachoratibu na kusimamia

masuala ya Wanawake kwa kuwa na idara au dawati la wanawake kwa kila chama cha ushirika nchini.


Bw. Malunde alieleza Kongamano hilo kuwa utayari na kujiamini kwa Wanawake wajasiriamali katika kukopa nako ni sehemu ya changamoto zilizopo katika Vyama vya Akiba na Mikopo. Akitolea mfano Katika utafiti uliochapishwa na shirika la kazi duniani (ILO) mwaka 2014 unaonyesha kuwa zaidi ya 80% ya maombi ya mikopo ilitengwa kwa ajili ya wajasiriamali wanawake na 90% iliiva kwa ajili ya kuwapatia wanawake, lakini ni 18% ya wanawake wajasiriamali ndio walioomba mikopo hiyo na 28% walioomba katika taasisi nyinginezo za kifedha.

"Takwimu zinaashiria kuwa sio tatizo la kuwepo kwa fedha isipokuwa ni masuala mengine kama vile riba na masharti magumu kama chanzo kikuu cha wanawake kushindwa kukopa," alieleza Naibu Mrajis Malunde.



*Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Akiba na Mikopo (SCCULT), Bi. Somoe Nguhwe akieleza jambo wakati wa Maadhimisho Kuelekea Siku ya Kimataifa ya Vyama vya Akiba na Mikopo Duniani, Jijini Arusha*

Kwa Upande wake Makamu Mwenyekiti wa Muungano wa Vyama vya Akiba na Mikopo nchini (SCCULT) Somoe Nguhwe katika Kongamano hilo amewataka Viongozi wanawake katika Vyama vya Akiba na Mikopo kutumia nafasi zao za uongozi kuhamasisha, kutoa elimu na fursa za kuwaandaa wasichana kuwa viongozi. Makamu huyo alisistiza kwamba ni muhimu Wanawake kuingia kwenye Uongozi kwani nafasi ya Mwanamke kwenye jamii ni kubwa na muhimu hususani kama mlezi na msingi wa familia, Jamii na Taifa kwa ujumla.


USHIRIKA
KWA
WOTE

www.ushirika.go.tz ushirika@ushirika.go.tz ushirika_tcdc

@ushirika_tcdc Tume ya Mendeleo Ushirika

***"Ushirika - Pamoja Tujenge Uchumi Imara na Endelevu"***